






## MATUMIZI YA NAMBARI ZA ISBN

Kama zilivyo bidhaa nyingine za viwandani, ambazo hutambulishwa kwa namba maalumu yenye msimbo milia (Bar Codes), pia vitabu hutumia namba maalumu iitwayo ISBN ambayo hupewa msimbo milia wake (Bar Codes).

## MACHAPISHO YANAYOSTAHIKI

- ➤ Kitabu (Printed books and pamphlets).
- ➤ Vitabu vya nukta nundu (Braille publications).
- ➤ Vitabu vya sauti vilivyobadilishwa kutoka kwenye maandishi halisi (Audiobooks or talking books).
- ➤ Vitabu vya kielektroniki (E-Books).
- ➤ Video, filamu na miundo ya kimtandao ambayo inahusika moja kwa moja na masuala ya utoaji wa maelekezo na elimu tu.
- ➤ Vitabu vya Sanaa ya uchoraji.

## UTANGULIZI

Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar, inatoa huduma ya **ISBN** na **ISSN** kwa waandishi na watunzi wa vitabu walioko Unguja na Pemba (**Zanzibar**).

### MAANA YA ISBN

**ISBN** ni ufupisho wa maneno ya kiingereza ambayo ni **International Standard Book Number**, ni nambari yenye tarakimu kumi na tatu (**13**) ambayo hutumika kama kitambulisho cha kipekee kinachotumika kimataifa kwa vitabu.

ISBN 978-0-7334-2609-4

9780733426094

## WAHUSIKA WANAOPASWA KUPATIWA ISBN

- ➤ Wachapishaji.
- ➤ Wauzaji wa vitabu.
- ➤ Maktaba mbali mbali.
- ➤ Watumiaji wa kimtandao.
- ➤ Wanaojishughulisha na usambazaji wa bidhaa za vitabu kwa ajili ya uagizwaji.

## GHARAMA ZA KUPATIWA HUDUMA YA ISBN

Uwanachama wa **ISBN** hutolewa kwa gharama ya **Tshs 30,000/=** sambamba na kupatiwa namba moja ya **ISBN**. Hivyo kila mwanachama atachangia **Tshs 5,000/=** ya kujaza fomu kwa kila anapohitaji **ISBN** mpya.






## MAANA YA ISSN

**ISSN** ni kifupi cha (International Standard Serial Number) ni nambari yenye tarakimu 8 inayotumiwa kutambua magazeti, na majarida ya kila aina, yanayochapishwa kwa karatasi na ya kielektroniki.

ISSN 1144-875X

9 771144 875007

## MATUMIZI YA NAMBA ZA ISSN

Matumizi rasmi ya ISSN ni utambuzi wa chapisho, ili chapisho liweze kutambulika kitaifa na kimataifa ni lazima liwe na nambari hizi.

## MACHAPISHO YANAYOSTAHIKI

- Magazeti.
- Machapisho ya mwaka (Reports, Directories, Lists, etc).
- Majarida (Journals, Magazines).
- Tovuti.
- Kanzidata (Database).
- Blog.

## MAWASILIANO:


| +255 776 792 299

| www.zls.go.tz

| Maisara - Zanzibar

| @maktaba_zanzibar


HUDUMA ZA MAKTABA · LIBRARY SERVICES · ZANZIBAR

# BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR




# MUONGOZO WA UTOAJI NA UTUMIAJI WA NAMBARI ZA ISBN NA ISSN